

WIMBO WA NISHATI

Chorus

Nishatii mbadala, aaa aaah!

Ni yetuu sisi sote, Tuitumie (eee!!) x 2



Ukombozi umeshakuja fungua mboni uonee,
Usiwaze tena kuhusu kuni kuna majiko janja mamaa,
Moshi wa mafiga matatu, unamadhara mengi mamaa
Ugonjwa wa kifua kikuu, mafua yasiyo isha ee!



Tumia jiko janjaa, wala halina moshi sanaa
Kwa kutumia ukuni mmoja, unapika mboga na wali
Achana na vibatari, anza kutumia solar taa,
Hutumia nguvu ya jua, sio mafuta ya taa,
Ina mwanga mkali sanaa inachaji pia na simu ee!

Chorus

Nishatii mbadala, aaa aaah!

Ni yetuu sisi sote, Tuitumie (eee!!) x 2

Karibu kituoni, (uuh!) Kituo cha nishati,



Kilicho Donyo sambu, na kingine Olkung'wado,

Utapata huduma hizoo, kwa wahudumu wetu hapoo

Ulizaa maswali yotee, yahasuyo nishati ujibiwe.



Uzindikaji wa mbogamboga, kwa kutumia mwanga wa jua,

Utengenezaji sabuni, kwa mimea yetu asili,

Shukurani kwa Oikos, kitengo cha nishati,

Jiko janja, Sola pawa, mbogamboga na sabuni,

Oikos rafiki kwa wanakijiji wote eh, eh!!



Chorus

Nishatii mbadala, aaa aaah!

Ni yetuu sisi sote, Tuitumie (eee!!) x 2



OUTRO

Cheza nami yoo, (uuuhuu!!)

Kwa pamoja, (yeah)

Ah, ah, ah, ah.....Nishati

